

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



For Competitive, Efficient, Quality and Safe Transport Services

Surface and Marine Transport Regulatory Authority
Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini

TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA YA MKUTANO WA KUKUSANYA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA VIWANGO VYA NAULI ZA TRENI YA MJINI KATIKA NJIA YA DAR ES SALAAM – PUGU YALIYOWASILISHWA NA KAMPUNI YA RELI TANZANIA (TRL)

Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) imepokea maombi ya viwango vya nauli za treni ya mjini kati ya kituo cha Dar es Salaam na Pugu. Maombi yamewasilishwa na Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) ambayo ndiyo itatoa huduma hiyo.

Viwango vya nauli vinavyoombwa ni vifuatavyo:

Na	Maelezo	Nauli inayopendekezwa (TZS)
1	Mtu Mzima	600.00
2	Mtoto au Mwanafunzi	200.00

Kwa kuzingatia Kifungu Na. 18 cha Sheria ya SUMATRA, Mamlaka imeandaa Mkutano wa kukusanya maoni ya wadau katika Ukumbi wa Karimjee tarehe 11 Agosti, 2016. Mkutano utanza saa 3.00 asubuhi.

Mamlaka pia itapokea maoni ya maandishi kuhusu maombi haya. Maoni ya maandishi yanaweza kuwasilishwa katika mfumo wa barua pepe kupitia tariffviews@sumatra.go.tz au kuwasilishwa katika ofisi za Makao Makuu ya SUMATRA zilizopo kona ya Barabara ya Ali Hassan Mwinyi na Mtaa wa Nkomo Jijini Dar es Salaam. Maoni pia yaweza kutumwa kwa: Mkurugenzi Mkuu, SUMATRA, S.L.P 3093, Dar es Salaam. Mwisho wa kupokea maoni ya maandishi ni tarehe 19 Agosti, 2016.

Imetolewa na

**Mkurugenzi Mkuu,
SUMATRA**